Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

**Kikao cha Nane – Tarehe 5 Februari, 2009**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, leo ni siku ya Alhamisi tunaanza na Maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, itabidi nitafute miwani mingine ya kuonekana zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Rais, alikuja katika Mkutano wa Kumi na Mbili (12)kulihutubia Bunge na akaahidi kwamba fedha ambazo zimelipwa za ziada katika mradi wa Rada ataiomba Serikali ya Uingereza iturudishie. Na kwa kuwa jana Bunge lako Tukufu lilipitisha mapato ya ziada kwa Serikali kutokana na mapato ya *EPA*.

Je, hatua ya utekelezaji kwa hii kauli ya Rais imefikia wapi? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu Ndugu yangu Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, swali lake zuri la leo kama ifuatavyo:- (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya sina *current position* ya suala hili lakini kwa taarifa nilizokuwa nazo mpaka muda mfupi uliopita hivi ilikuwa inaonyesha tu kwamba suala hili halijafikia tamati yaani uchunguzi wake bado haujakamilika na kwa maana hiyo siwezi nikajua kwa kweli kama umekamilika *then what steps should be taken* kulingana na hilo swali ulililoiuliza. Lakini nikapata muda tunaweza tukalifuatilia zaidi kidogo baadaye tukakupa labda maelezo ya uhakika.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kwa mujibu wa taarifa za uchunguzi ni kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali, alishapewa taarifa ya uchunguzi mwaka mmoja uliopita juu ya jambo hili na katika taarifa hiyo ya Uchunguzi yametajwa majina na akaunti za watu ambao wanahusika na hizo fedha. Je, Serikali kwa nini isitumie utaratibu ule ule wa *EPA* uliowaambia watu warudishe fedha, wakarudisha na hatimaye leo Bunge likapata nafasi ya kuzipeleka katika kilimo na kwa sababu akaunti zinajulikana, watu wanajulikana kwa nini utaratibu huo usitumike zile fedha sasa zikarudi nchini? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sidhani kama ni tatizo kubwa kama unayoyasema yatathibitika kwamba ndiyo hali halisi. Lakini ninachochelea kusema tu ni kwamba wewe mwenyewe umekuwa ukiona hata kwenye vyombo vya habari inaonekana jambo hili bado linafukuta kwa maana ya kwamba hatujafika mahali *concrete* tukasema jambo limemalizika vizuri na kwa hiyo, tuweze kuchukua hatua zinazostahili.

Kwa hiyo, mimi nina hakika kama tutafikia tamati, mwisho wa zoezi hili na kwa mambo haya ambayo tunatamani yafanyike ikaonekana yanawezekana kwa mujibu wa taratibu zetu, mimi sioni kama kutakuwa na ugumu hata kidogo. Ni suala tu la kufanya subira kidogo. (*Makofi*)

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mtikisiko mkubwa ulizozikumba nchi tajiri duniani ambao umepelekea makampuni makubwa kufilisika katika nchi hizo na kwa kuwa madhara yake tumeanza kuyaona hapa nchini kwa kukosa soko, katika soko la dunia baadhi ya bidhaa kama pamba, katani, *Tanzanite* na dhahabu. Sambamba na hilo shilingi yetu inazidi kushuka thamani mbele ya fedha za kigeni. Mfumuko mkubwa wa bei lakini vile vile tayari wafanyabiashara hapa nchini wameanza kuyumba na hali hii. Je, Serikali imejipanga vipi kunusuru uchumi wa Watanzania na Taifa kwa ujumla na hali hii tete?

**NAIBU SPIKA:** Ingawa nafahamu kuna mkutano baada ya kipindi hiki na kwa kuwa suala lenyewe ni zito Waziri Mkuu naomba ujaribu kujibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Suala alilouliza ndugu yangu Mbunge wa Meatu ni pana sana. Ningeweza nikajaribu kutoa maelezo kuhusiana na jambo hili. Lakini nilifikiri kwa kumsaidia nadhani ile semina ambayo Gavana wa Benki Kuu, anakuja kuitoa itaonyesha kwa undani matatizo yalivyo makubwa na hatua ambazo tulimshauri, atushauri kama Serikali ili tuweze kuona namna gani tutaweza kukabiliana na hali hiyo. Kwa hiyo, siwezi kwa kweli kujaribu kusema vitu ambavyo pengine sina uhakika navyo. Lakini mimi nifikiri tukisubiri wote hiyo semina itatusaidia sana kuweza kujua hali ilivyo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante nakwenda kufuatana na *gender*.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ongezeko la wanafunzi wa Elimu ya Juu na vyuo vyake ikiwemo Dodoma tunalihitaji liwe endelevu na wakati huo huo linaashiria ongezeko la mapato na matumizi katika Bajeti yetu. Na kwa kuwa mpango huo wananchi wengi wa Tanzania wanalipongeza na kutoa shukrani za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania na Serikali yake ya Chama cha Mapinduzi. Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu, utakubaliana nami kwamba iko haja ya kuongeza au kupanua wigo wa ukusanyaji wa fedha kwa ajili ya kuendeleza mpango huo na kama ndivyo ni mipango gani angalau michache ambayo tayari imeshaanza kufanyika?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge, asilimia 100 katika hilo ambalo amelisema. Lakini niseme vile vile kwamba jukumu kwa kweli la kujaribu kuona ni mbinu gani au tutumie mambo gani kupanua uwigo kwa maana ya kuongeza mapato yetu kwa bahati nzuri ni jukumu letu sisi wote.

Ila ninachoweza kusema ni kwamba katika Bajeti ijayo tutajaribu kama Serikali kuonyesha ni maeneo gani ambayo tumedhamiria kwa dhati kuyaongeza ili tuweze kupata fedha nyingi zaidi ili mpango huu kwa uhakika uweze kufanyika na kukamilika inavyotakiwa. Kwa sasa bado nadhani ni hatua za awali juhudi kweli zipo lakini nadhani kubwa ni lazima tutazame kwenye mpango wa Bajeti unaokuja.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa majibu yako mazuri.

Kwa kuwa nami ni mdau ukizingatia kwamba ni mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa kupitia Wazazi ambayo elimu ni kipaumbele, nimefanyia kazi na kuona kuna baadhi ya mikakati kama 13 ambayo ingetuwezesha kusonga mbele. Je, utakubaliana nami niilete kwako ili uweze kuunganisha pamoja na mipango mingine na unipangie muda ili niweze kuifafanua? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, mama nakushukuru tuletee. (*Makofi*)

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mheshimiwa Waziri Mkuu tulishuhudia mchakato wa uchaguzi wa Kenya na Zimbabwe hivi karibuni na matokeo ya watawala kukataa uamuzi wa wananchi. Lakini pia tumeona hivi karibuni mwezi mmoja, miwili nyuma mchakato wa Uchaguzi wa Ghana, ambao ulikuwa ni wa haki, huru na amani, ambapo uamuzi wa wananchi ulikuwa ni kuwaweka Wapinzani katika Serikali na pametokea kubadilishana madaraka kwa njia ya amani. Nakuja ninyi siyo Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mimi ndiyo Naibu Spika hapa.

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, Tanzania inaelekea kwenye uchaguzi mwaka unaokuja. Je, unahisi Serikali yetu, viongozi wake na Tume

zake za Uchaguzi zijifunze nini katika aina mbili hizi za uchaguzi? Halafu la pili, Mheshimiwa Waziri Mkuu, iwapo wananchi wataamua kuwaweka Wapinzania madarakani. Je, unahisi Serikali/Chama Tawala kitakubali uamuzi huo? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Swali la pili, Mheshimiwa Waziri Mkuu, usijibu unajibu la kwanza.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu Ndugu yangu Mheshimiwa Dr. Ali Tarabu Ali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, namwomba tu Mheshimiwa Mbunge fanya subira una haraka gani baba, subiri tu! Lakini nataka tu niseme kwa uhakika kabisa kwamba nchi hii ni moja kati ya nchi chache sana ambazo tunajitahidi sana kuheshimu utawala bora.

Ni moja kati ya nchi chache sana ambayo tumeonyesha mfano mzuri katika kujenga demokrasia hasa ya vyama vingi. Kwa hiyo, mimi naamini kabisa kama mtabahatika kupata hilo unaloliombea basi *well and good* nchi itasema kila la heri. Lakini uwezekano ni mdogo kweli. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kumwuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza, awali napenda kuipongeza Serikali kwa juhudi zake kubwa inazofanya za kuboresha elimu katika nchi yetu na kuhakikisha kwamba hata kila mwenye uwezo wa kwenda shule aweze kwenda shule. Hii ni pamoja na kuwalipia karo/gharama zote za wale wanafunzi ambao wazazi wao hawana uwezo wa kuwasomesha.

Lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na juhudi hizo nzuri na kubwa zinazotolewa na Serikali, bado kuna kero kubwa ambayo imejitokeza kwa hawa wanafunzi wanaomaliza darasa la saba na kufaulu kwenda sekondari, kwani hadi leo tunavyozungumza katika Jimbo langu la Musoma, lakini vile vile katika maeneo mengine wale wanafunzi waliofaulu kwenda sekondari huku hawana uwezo ambao Serikali iko tayari kuwalipia hadi sasa hawa wanafunzi wako majumbani kwa sababu Serikali bado haijapeleka fedha za kuwalipia. Ningependa kufahamu Serikali inalifahamu hilo na sasa inasema nini kuhusiana na mpango huo?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijaribu kutoa maelezo kidogo kuhusiana na swali la Mheshimiwa Vedastus Manyinyi. Analolisema linawezekana lakini kwa upande mmoja linatokana na Halmashauri zetu kutokuwa na mfumo mzuri sana namna ya kushughulikia jambo hili, tumelieleza mara nyingi lakini inabidi tuendelee kulisema. Tulishawatahadharisha Halmashauri zote kwamba mnapokuwa katika mchakato wa mitihani ya darasa la saba, lakini kabla hamjafikia ni vizuri mkawa na maoteo ya kuwawezesheni kujua angalau idadi kiasi ya wanafunzi wanaweza wakachukuliwa katika kidato cha kwanza.

Hii ingewawezesha kwa uhakika zaidi kuweza kuwa na viwango vya matarajio ya fedha ambazo tunaweza tukazipata. Lakini hawafanyi hivyo kwa hiyo wanangoja mpaka matokeo yametoka halafu ndiyo wanaanza kuhangaika kutafuta fedha. Hiyo haiwezekani. Lakini kwa sababu umeuliza ni jambo jema, ni jambo zuri acha tutalishughulikia tuone kama tunaweza tukalipatia ufumbuzi wa haraka. (*Makofi*)

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niulize swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu tumekumbwa na tatizo kubwa sana la maji nchini. *(Makofi)*

Katika baadhi ya sehemu mbali mbali pamoja na jitihada za Serikali za kuleta miradi ya *Quick wins*, za kuleta miradi ya Ziwa Victoria, katika sehemu zile za *Lake Zones* na miradi mbalimbali ya *World Bank* kama Lindi, lakini bado tatizo la maji nchini kwa kweli ni kubwa sana hasa hasa katika eneo la Nachingwea, Lindi Mjini na baadhi ya mikoa kama Singida sijui Shinyanga na Tabora.

Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali sana tunaomba tujue ni mikakati ipi imewekwa kwa ajili ya kutatua tatizo hili la maji nchini. (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Fatma Mikidadi, kwa asilimia kubwa kwamba tatizo la maji ni kubwa sana hapa nchini na kwa sehemu kubwa linatokana na uwekezaji mdogo katika sekta ya maji. Kwa upande mwingine ni ongezeko kubwa sana la wakazi kwa maana ya Watanzania wamezaliana kwa wingi, ongezeko haliwiani na kiwango cha uwekezaji katika sekta hiyo.

Lakini vilevile hata ile miundombinu ambayo tulikuwa tunayo tukadhani ingetosheleza, sehemu kubwa ya miundombinu hiyo kama visima, pampu nayo kwa sehemu kubwa imeharibika na wakati mwingine tutachukua muda mrefu sana kuikarabati.

Sasa swali lake ni nzuri sana kwa hiyo tuna mikakati gani ili tuweze kuondoka hapa tulipo. Sasa tulikuwa tumejipa matumaini makubwa sana na miradi ya Benki ya Dunia. Lakini wote ni mashahidi, miradi hii ina mchakato mrefu na wakati mwingine haitoi matumaini makubwa sana ya kutatua tatizo hili.

Mimi kimtazamo na nataka niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwamba katika Bajeti inayokuja, tusiweke nguvu sana katika programu ambazo zinatokana na ufadhili ambao kwa kweli michakato yake ni mirefu. Tuamue katika Bajeti inayokuja katika maeneo ya vipaumbele tutoe nafasi kubwa sana kwenye sekta ya maji ili tuweze kupunguza tatizo hili kwa kiasi kikubwa. Vinginevyo tatizo hili litachukua muda mrefu kumalizika. (*Makofi*)

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana napenda kutoa shukrani kwa kupata nafasi hii na mimi niweze kumwuliza Mheshimiwa Waziri

Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kabla hutujapata uhuru tulikuwa na *province* nane, moja wapo katika Makao Makuu ya *Southern Province,* Lindi ilikuwa moja wapo.

Lakini Lindi ilizaa Ruvuma, Lindi ilizaa Mtwara na ikazaa mpaka Njombe, ilikuwa katika Mkoa wa Lindi. Bahati nzuri tumejitahidi Mkoa wa Lindi, kupitisha katika *RCC* na sehemu zingine tunahakikisha kuwa sehemu zile ambayo ilikuwa inatakiwa tuongeze tumeshaongeza na mpaka sasa hivi hatujapata Manispaa.

Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu, unatuambia nini wananchi wa Lindi ili tuweze kujua. Je, Manispaa tutaipata au tuna mikakati gani mizuri ya kuhakikisha na sisi Lindi tunanufaika na Manispaa?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba analolisema dada yangu Mheshimiwa Lulida, hata mimi ningetamani liwezekane kwamba Lindi siku moja iamuliwe kwamba ni Manispaa kama ninavyotamani Dodoma kuwa Jiji.

Lakini maamuzi hayo kwa sehemu kubwa yanategemea kama mmekidhi vigezo vya msingi ambavyo vinatakiwa vitekelezwe. Kwa bahati mbaya sana. Lindi kwa maana ya vigezo na hasa kigezo kikubwa cha uwezo wake wa kiuchumi bado wako chini sana na ili Manispaa iweze kumudu heshima ya kuwa Manispaa ni lazima muwe na uwezo wa mapato ya kutosha kuweza kujiendesha kwa sehemu kubwa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ninachoweza kusema tu kwa Mheshimiwa ni kwamba si kwamba Lindi haiwezi kuwa Manispaa hapana, itakuwa. Lakini lazima juhudi za kuongeza mapato kwa mbinu mbalimbali na njia mbalimbali ziongezwe ili tuweze kufika mahali na kuona kwamba sasa nadhani Lindi iko tayari kwa ajili ya kuwa Manispaa hatuna sababu ya kuwakatalia kwa sababu ni mfumo mzuri na mkiingia kwenye Manispaa iko miradi mbalimbali ambayo inajikita katika maeneo haya ya miji badala ya maeneo ya vijijini.

Kwa hiyo, ni jambo jema na mimi nasema tuendelee kujaribu kufanya kazi kwa juhudi zaidi. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Najua Mheshimiwa Waziri Mkuu analitegemea swali hili, tarehe 29 Januari, 2009 katika Wilaya ya Kilosa Serikali imeendesha *operation* ya kukamata ng'ombe. Wapiga kura wangu ambao wana Ndugu zao hapo, walinipigia na baadaye mimi mwenyewe nimetuma watu kwenda kuangalia, ng'ombe walikamatwa tarehe 29 Januari, 2009 wakazuiliwa kunywa maji, wakazuiliwa kuchunga, na wakaambiwa kwamba kuwatoa ng'ombe zao ni lazima walipe Shilingi 30,000/= kwa kichwa, na walipe Shilingi 5,000/= kwa kichwa kila ng'ombe akiwa chini ya ulinzi wa Polisi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa John Cheyo, swali sasa.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Sasa swali, kwa kuwa inavyoonekana huu msako sio wa Kilosa tu na sehemu zingine kama Ihefu umefanyika kwa hasara kubwa kwa wafugaji Waziri Mkuu, anaweza sasa akatueleza mapema kuwa kwamba msako huu utaendelea

mpaka Wilaya gani ili tuwaandae watu wetu kutafuta mahali pengine pa kuchunga hata kama ni kwenda Zambia au *Mozambique* ili watu wakimbie uharamia wa Serikali waliyoichagua. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu kwa heshima nimjibu Mheshimiwa Cheyo, kwanza hakuna uharamia wowote hakuna, kwa sababu nadhani swali la msingi hapa Mheshimiwa John Cheyo ni kwamba ninyi wachungaji wa ng'ombe mna utaratibu huu wa kutembeza ng'ombe usiku na mchana nchi nzima mpaka lini? (*Makofi*)

Ndiyo kwa sababu mlikuwa Shinyanga, mmeharibu mazingira, mmekuja Rukwa mmekwenda wapi, nauliza hii sio namna bora ya ufugaji hata kidogo na bahati mbaya sana mnapozunguka katika maeneo haya hamjali kama eneo hili ni eneo tengefu hamjali kwamba eneo hili ni *National Park*, hamjali kama eneo hili ni mmevuka mpaka Zambia mkarudishwa kwa nguvu.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani kama Taifa tukaendelea na aina hii ya ufugaji. (*Makofi*)
Kwa hiyo, Mheshimiwa John Cheyo, unalolisema ni kweli lakini wewe ni shahidi, ng'ombe tulio nao jamani ni wengi sana katika maeneo mengi ukilinganisha na uwezo wa malisho tuliyo nayo.

Mimi natoka Rukwa, na asilimia kubwa ya ng'ombe pale ni kutoka kwa Ndugu zangu shemeji zangu Wasukuma, ni wengi mno na sisi tumefika mahali Mkoa wa Rukwa tumesema jamani sasa (*enough is enough)* wametosha. (*Makofi*)

Sasa tukishasema hivyo, maana yake ni kwamba lazima watafute eneo jingine na huko mkiambiwa *it is enough* mtafute eneo jingine aah wapi!

Sasa, Kilosa kumetokea nini? Kilosa wafugaji hawa wameingia tena bila utaratibu, Kilosa wamejikuta wana ng'ombe wengi zaidi kuliko idadi waliyokuwa wameitarajia zaidi ya ng'ombe 100,000 ni zaidi ya kiwango ambacho kinachoweza kubeba malisho.

Kwa hiyo, ndiyo maana Halmashauri ikakaa chini ikasema hapana. Hili jambo lazima tushughulike nalo. Lakini ilikuwepo sababu nyingine ya msingi. Tatizo la wafugaji na hasa Ndugu zangu nyie Wasukuma mnapoamua kwamba ng'ombe lazima ashibe hamjali kwamba kama ni shamba la mkulima au hapana. (*Makofi*)

Hili nalizungumza *from my experience* mnalisha ng'ombe mpaka kwenye mashamba na ndiyo maana kuna ugomvi kati ya wafugaji na wakulima. Hata mkitengewa maeneo ya wakulima bado mnaona haiwezekani.

Kwa hiyo, Kilosa waliamua kwenye Baraza la Madiwani, wakatenga maeneo matatu ambapo wameamua ni vituo kwa ajili ya kukamata ng'ombe na kuwaweka. Ni

kweli wamekamata karibu ng'ombe 6,000, na ni kweli vilevile walitangaza kwamba tunaomba mifugo iliyoingia hapa ndani kinyume cha utaratibu hamkukaribishwa na vijiji husika iondoke.

Muda ulipofika Halmashauri ikasema lazima tukaze uamuzi wa Baraza. Ye yote ambaye atakaonekana hakutekeleza lile agizo anatozwa faini ya Shilingi 30,000/=. Hiyo ni faini ya mara moja. Wanakamata ng'ombe. ni kweli wanaweka katika vile vituo. Walisema ng'ombe wasikae pale kwa zaidi ya siku tatu na kila siku tutakutoza Shilingi 5, 000/= kwa kila ng'ombe, ni kweli.

Hakuna ng'ombe ambaye amekaa pale katika vituo vile vitatu kwa zaidi ya siku tatu. Mimi nakwambia ndiyo taarifa niliyopewa. Waliobaki zaidi ni mbuzi na kondoo ndiyo wamezidisha kidogo zaidi ya siku tatu.

Sasa katika mazingira haya Mheshimiwa Cheyo, ninachosema nimeona wanasheria wako wametuandikia barua wameamua kutoa *notice* kwa Halmashauri kwamba tutawashitaki vyema. Mimi nafikiri nao ni mkondo mzuri vilevile tuendelee nao waishitaki Halmashauri tuone itaishia wapi. Lakini mimi ninachosema kwamba kwa aina hii ya ufugaji kweli kabisa lazima tushirikiane tupate njia bora zaidi ya ufugaji. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cheyo naomba swali la nyongeza liwe fupi sana.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali hii iliyochaguliwa na wananchi ilisema kwamba itaboresha maisha yao kwa kupunguza umaskini wao na kwa kuwa nchi hii ni asilimia 4 tu ndiyo tunaitumia na asilimia 8 juzi tumegawa kwa wanyamapori.

Hivi ni kweli mantiki yako Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwamba hakuna utaratibu ambao unaweza ukafanywa watu wakatengewa maeneo katika nchi yetu ambapo wachungaji wakaendelea kuwa na mifugo yao kuliko kwa sasa hivi unachofanya ni kuwaua wale mifugo?

Pia kuwashurutisha hawa watu wauze hiyo mifugo kwa sababu unawaambia ondoka. Hujawaambia waende wapi na wasiende wapi, wakikanyaga waende siyo baskeli waende kwa magari huu ni ubinadamu kweli? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa John Cheyo, inakuwa hotuba Mheshimiwa.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, najua mnapofikia kwenye eneo la ng'ombe na mkulima ni lazima itakuwa *very sensational.* Lakini ninachosema tu ni kwamba mimi nafikiri tukae chini wote pamoja tujaribu kutafuta suluhu la tatizo hili. Wakulima wanaathirika na mimi nataka kusema kwamba tena wanaathirika zaidi katika mazingira ninayoyajua mimi kuliko hata mfugaji.

Maana ukisema hamsemi waende wapi na mimi nasema kwani walitoka wapi?

Kuna namna nyingi za kujibu swali hili ndio maana nimesema *bottom line* tukae chini tujaribu kutafuta njia bora zaidi ya kuwasaidia hwawa wafugaji. Lakini kubwa katika hili ninachoweza kusema tu ni kwamba kwa maelezo niliyopewa Mzee Cheyo, maana mimi ilibidi nizungumze baada ya kuona barua yako, katika vituo hivyo vitatu unavyovisema hakuna ng'ombe hata mmoja aliyekufa, hakuna. Na wala si kweli kwamba eti hawakunywa maji, hawakuchungwa, si kweli. Ndio wewe umeletewa malalamiko ya maandishi na mimi nimezungumza na viongozi. Ndio maana nimesema pengine mkitaka ukweli watie moyo wapeleke jambo hili Mahakamani ndio suluhu ambayo utaweza kuipata. *(Makofi).*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati wa Maswali kwa Waziri Mkuu umepita. Mheshimiwa waziri Mkuu, naomba nikushukuru kwa kuweza kujibu maswali yote. *(Makofi)*

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68 (7). Kipindi cha Maswali ya Waziri Mkuu, Spika alitoa maelekezo na utaratibu wa namna ya watu kuuliza maswali kwa maana ya kuwahi siku ya maswali. Kwa kuwa orodha iliyosomwa leo ni tofauti kabisa na orodha ambayo ilikuwa katika Ofisi ya Katibu leo asubuhi, ambayo mimi nilikuwa ni miongoni mwa watu waliofika pale saa 11.45.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba mwongozo wako kwamba kuna utaratibu gani ambao Mwongozo wa Spika umevunjwa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Inadhihirisha kwamba jana jioni hukuwepo hapa; kwa sababu tangazo tulilotoa hapa kwamba watu wanaofika saa 11.00 hawapokelewi tunaanza saa 1.30 ndivyo ilivyotangazwa jana.

Pili, ukiangalia nilivyopitia orodha hii, nimezingatia Vyama karibu vyote isipokuwa nilipofika *CHADEMA, UDP* akatumia dakika 10, kwa hiyo hukufikiwa lakini ulikuwa unafikiwa manaake nimeenda *CHADEMA, CUF, CCM, gender,* na eneo.

Lakini nilipofika eneo lile sasa mwenzetu Mheshimiwa John Cheyo, akatumia dakika 10, kwa hiyo ikashindwa kukufikia, lakini huo ndio ulikuwa ni mpangilio. Tunaendelea, Katibu. *(Makofi)*

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni ya 68, nilikuwa naomba kupata Mwongozo wako. Kati ya maelekezo yako kama Naibu Spika, na maelekezo ya Spika, ni yapi yafuatwe?

Kwa sababu Spika, alitufahamisha humu Bungeni kwamba anayewahi, wewe jana umetangaza tofauti kabisa na maagizo ya Spika; tufuate maamuzi yepi, yako au ya Spika? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zitto, najua daima ni kutaka kugonganisha mtu na mtu. Sasa nakuambia maelekezo ni yale yatakayotolewa hapa ndani na maelekezo ya mwisho ndiyo yanayofuatwa kuliko yale yaliyotangulia na ya mwisho ilikuwa ni saa 01:30, Katibu. *(Makofi)*

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Katika Maswali ya kawaida tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu; Mheshimiwa Cassian Kayombo, ndio atauliza swali la kwanza.

Na. 97

### Kujenga Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mbinga

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO** aliuliza:-

Je, ni mwaka gani wa fedha Serikali itaanza kujenga Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, pamoja na makazi yake katika Wilaya ya Mbinga?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, Mbunge wa Mbinga Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jengo linalotumika hivi sasa kwa ajili ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mbinga na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya lilijengwa kwa ajili ya Makao Makuu ya Wilaya ya Mbinga. Baada ya Serikali kurudisha Mamlaka za Serikali za Mitaa, Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga iliomba vyumba katika jengo hilo kwa ajili ya matumizi ya Ofisi. Jengo hilo limeendelea kutumika kwa ushirikiano kati ya Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Mbinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkutano wa 13 wa Bunge lako Tukufu nilijibu swali Namba 87 linalofanana na swali hili kutoka kwa Mheshimiwa Kapteni John Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mpunguze minong’ono tumsikilize.

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilitoa ushauri kwamba iwapo Ofisi ya Mkuu wa

Wilaya ya Mbinga inaona kuwa kuna haja ya majengo mengine yajengwe zaidi ya hayo yanayotumika, sasa ione uwezekano wa kuweka kwenye vipaumbele vya Bajeti kwa mwaka ujao wa Fedha.

Nilifikisha ushauri huu kwa barua yenye Kumb.Na.AB.231/403/01 ya tarehe 6 Novemba, 2008 ambayo Mheshimiwa Kayombo pia alipata nakala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nyumba ya Mkuu wa Wilaya, katika mwaka wa Fedha 2008/2009 kiasi cha shilingi milioni 200 zilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya Mkuu wa Wilaya ya Mbinga.

Fedha zote zilizotengwa kwa kazi hiyo zimepelekwa kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma na tayari zimepokelewa. Utekelezaji wa mradi huo hivi sasa uko katika hatua za awali ambapo Zabuni ilitangazwa na sasa shughuli ya upembuzi zabuni, *evaluation,* imekamilika. Bodi ya Zabuni inakaa leo tarehe 05 Februari, 2009 kwa ajili ya kupitia mapendekezo ya Timu ya Tathmini hatimaye kutangaza Mkandarasi atakayeshinda kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa. Kazi ya ujenzi itaanza mara moja baada ya kumpata Mkandarasi atakayeshinda.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni lazima niishukuru Serikali kwa kazi hii nzuri ambayo imeifanya ya kutenga fedha milioni 200 kwa ajili ya nyumba ya Mkuu wa Wilaya ya Mbinga. Sasa sambamba na kazi hii nzuri kwa kweli sina swali isipokuwa nina ombi kwamba sasa Mheshimiwa Naibu Waziri, yupo tayari kutusaidia kuwaandikia hawa watendaji katika Mkoa na Wilaya kwamba Wabunge wa Mbinga wakiwakilisha wananchi wao wanaomba Mkuu wa Wilaya ya Mbinga ajengewe Ofisi.

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa namshukuru kwa kushukuru kwamba amefurahishwa na majibu na mpaka ninavyokuja hapa tumezungumza na Mbinga, tumezungumza na Mkurugenzi Mtendaji na tumezungumza pia na Mkuu wa Wilaya. Hivi tunavyozungumza eneo kwa maana ya ardhi ambayo itajengwa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya imeshapatikana, ukweli ulivyo ni kwamba hali ilivyo pale sasahivi kitakachotakiwa kubakia pale ni Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga na sio Ofisi ya Mkuu wa Wilaya. Kwasababu Ofisi ya Mkuu wa Wilaya mahitaji yake ni madogo sana kwa maana ya nyumba. Hawa wamekuwa wanashirikiana vizuri, wamefanya kazi kwa pamoja hakuna mtafaruku wala ugomvi wowote.

Sasa kuhusu ombi hili la kuwaambia, mimi nimeshaanza na tayari nimezungumza nao na nimewaambia kwamba kuna haja ya kuhakikisha kwamba tunajenga Ofisi ya Mkuu wa Wilaya mahali pengine. Kwahiyo hilo tutatekeleza.

**MHE. IDD M. AZZAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tatizo la Mbinga linafanana kabisa na tatizo lililopo Dar-es-Salaam; na Kwa kuwa, Ofisi ya Mkuu wa

Wilaya ya Ilala ndiyo inayotumika kama Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar-es-Salaam. Je, ni lini Serikali itajenga Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar-es-Salaam?

**AIBU WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasahivi ni kweli kwamba kuna hilo tatizo ambalo Mheshimiwa Mbunge, amelizungumzia na kazi inayofanyika sasahivi ni ya kutafuta kiwanja kwa ajili ya kuhakikisha kwamba jengo hilo linajengwa kama anavyoshauri.

Na. 98

**Kujenga Barabara Kupitia Mpango wa MCC**

**MHE. OMAR ALI MZEE** aliuliza:-

Kwa kuwa, kuna ahadi ya kujenga barabara tano katika Kisiwa cha Pemba kupitia Mpango wa *Millenium Challenge Cooperation, MCC:-*

Je, mradi huo utaanza lini?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mbunge wa Jimbo ka Kiwani, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba barabara tano zenye jumla ya urefu wa kilometa 35, katika kisiwa cha Pemba zitajengwa kupitia mpango wa Marekani wa *Millenium Challenge Account (MCC).*

Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa kusimamia na kukamilisha taratibu mbalimbali za awali za matayarisho ya ujenzi wa barabara hizo ikiwa ni pamoja na utayarishaji wa nyaraka za Usanifu na Zabuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kukamilika kwa nyaraka za Usanifu na Zabuni, nyaraka hizo ziliwasilishwa *Millenium Challenge Cooperation, MCC,* mwezi Juali, 2008 kwa ajili ya mapitio. Baada ya mapitio ya kina, wataalamu wa *MCC* wameeleza kuhusu kuwepo kwa mapungufu ambayo kulingana na miongozo ya mfuko huo yanahitaji kufanyiwa kazi zaidi, ili kuweza kufikia vigezo na viwango vilivyowekwa na *MCC.* Zoezi hili litakapokamilika, hatua ya kuitisha zabuni za ujenzi zitafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omar Ali Mzee, kwa kutoa mtiririko wa mpangilio wa shughuli mbalimbali za mradi zitakavyo kwenda kama ifuatavyo:-

1. Kuitisha zabuni za upembuzi yakinifu na usanifu ili kupata Mhandisi Mshauri; Zoezi hili limeanza na litakamilika kati ya Januari mpaka Juni, 2009.

2. Utekelezaji na ukamilishwaji wa kazi ya Usanifu na Nyaraka za Zabuni; Zoezi hili litafanyika kati ya mwezi wa Julai mpaka Januari. 2010.

3. Kupitishwa kwa Zabuni za Ujenzi na kukamilisha mchakato wa kumpata Mkandarasi; zoezi hili litafanyika kati ya Januari mpaka Mei. 2010.

4. Matayarisho ya Mkandarasi kuleta vifaa vya kazi yatafanyika kati ya mwezi Mei 2010, na hivyo kazi ya ujenzi kuanza Julai, 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kuwa barabara hizi zitajengwa. Wakati huo huo tunaendelea na mashauriano ya kitaalamu kuhusu uwezekano wa kufupisha baadhi ya muda uliokadiriwa kuhitajika ili angalau shughuli za ujenzi ziweze kuanza mapema zaidi.

**MHE. OMAR ALI MZEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba nimuulize swali moja tu la nyongeza. Je, ni barabara gani hizo tano zitakazojengwa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpatie orodha hiyo baada ya kikao hiki. *(Makofi)*

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake na mmoja kati ya wananchi wa Zanzibar wanaopenda sana maendeleo katika visiwa vile ni mimi. Lakini hivi karibubi kule Kisiwani Pemba kulijitokeza kikundi na kikatangaza kutaka kujitenga na Zanzibar, lakini unapojitenga na Zanzibar, maana yake unajitenga na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika sasa swali, Mheshimiwa naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba kwa kuhofia kikundi hiki kisije kikasambaza sumu hii ikaenea Kisiwa kizima cha Pemba, haoni kwamba itakuwa ni vizuri tukasitisha kwanza mpaka kikundi hiki kikatangaza kutokujitenga? *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mimi sijaelewa, swali linahusu barabara, kikundi kinahusiana nini hapa? Mheshimiwa Serukamaba. *(Makofi/Kicheko).*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa naibu Spika, miradi ya *MCC* iko nchi nzima moja ya sehemu ambako kuna mradi wa *MCC* ni katika mradi wa umeme wa Mkoa wa Kigoma. Nataka Naibu waziri aniambie kwa mradi huo sasa anao, ratiba ya utekelezaji ikoje?

**NAIBU SPIKA:** Nadhani suala lenyewe ni kwamba ile ahadi ya *MCC* imefikia wapi. Sio umeme wala nini? Naomba Mheshimiwa Naibu Waziri ujibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, pamoja na la kwako wewe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi ya kutekeleza miradi ya *MCC* ipo palepale na kama nilivyokuwa nikieleza siku za nyuma Bunge lako Tukufu, kwamba mradi huu wa *MCC* ambao unakaribia dola milioni 700 ni kwa kipindi cha miaka mitano. Na ndugu yangu Mheshimiwa Peter Serukamba ametaka *program* ya utekelezaji wa mradi wa umeme Kigoma, naahidi vilevile nitampatia kabla hatujamaliza Bunge hili.

**NAIBU SPIKA:** Nilijua majibu yangekuwa hivyo. Mheshimiwa Switi. *(Kicheko)*

**MHE. ELETTA N. SWITI:** Mheshimiwa naibu Spika, kwa kuwa taabu ya watu wa Pemba inafanana kabisa na taabu ya watu wa Rukwa kuhusu barabara. Na kwa kuwa, watu wa Rukwa wameshachoka kabisa na ahadi hii. Je, leo Serikali inaweza kutamka wazi ni lini basi na hawa watu wa Rukwa barabara ya kutoka Tunduma – Sumbawanga na Sumbawanga – Mpanda itajengwa?

**NAIBU SPIKA:** Mimi nilisema ajibu kuhusu mambo ya *Millenium Goals,* ukimwambia ajibu barabara hawezi sio mwenyewe. Kwa hiyo kuna mtu anaweza kujibu? Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Issa Kassim Issa.

**MHE. ISSA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya tarehe 25 mwezi wa pili, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa.........

**NAIBU SPIKA:** Uliza swali, uliza swali!

**MHE. ISSA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hili swali kulitoa.

Na. 99

**Ahadi ya Kukamilisha Njia ya Mtoni - Amani**

*(Swali lililotajwa hapo juu liliondolewa na Muuliza Swali)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Castor Raphael Ligallama, atauliza swali.

Na. 100

**Vyanzo Mbadala Vya Maji Kwa Miji Ya Ifakara Na Mlimba**

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ilikubali kuanzisha miradi ya kuipatia maji miji ya Ifakara na Mlimba, vyanzo mbadala vya maji kwa njia ya mtiririko, *gravity water*, ambapo mji wa Ifakara utapata maji toka eneo la Kiburubutu katika mto Lumemo na mji wa Mlimba kupata maji kutoka chanzo cha mto Mpanga:-

(a) Je, ni lini mpango huu utaanza?

(b) Kwa kuwa, hivi sasa chanzo cha maji katika miji hiyo ni visima vinavyotumia pampu za umeme. Je, Serikali itakuwa tayari kusaidia katika kulipia umeme unaotumika?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Castor Ligallama, Mbunge wa Kilombero lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa maji katika mji wa Mlimba unaendeshwa na kampuni ya watumiaji maji iliyoanzishwa mwaka 1998. Kupitia utekelezaji wa programu ya usambazaji wa majisafi na usafi wa mazingira vijijini, *RWSSP*, mji wa Mlimba umo kwenye miradi 10 iliyoteuliwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero kupata huduma ya maji kwa kutumia mto Mpanga. Mchakato wa kumpata Mtaalam mwelekezi atakayesanifu miradi hiyo umekwishaanza.

Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero tayari imepata ridhaa ya kuendelea na hatua ya kufungua mapendekezo ya kifedha ya kampuni zilizoomba kazi. Kinachofanyika na Halmashauri sasa ni kufanya tathmini ya mapendekezo hayo kutoka kwa kampuni zilizoomba. Matarajio yetu ni kwamba mtaalamu mwelekezi atapatikana mwezi Machi, 2009 na kuanza kazi mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma ya maji katika mji wa Ifakara inatolewa na Mamlaka ya maji ya mji wa Ifakara. Katika kuboresha huduma ya maji, uchunguzi na usanifu wa miundombinu ya maji utafanywa na Mhandisi Mwelekezi anayefanya kazi ya usanifu wa mradi wa maji wa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka mjini Morogoro.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mazungumzo yanazidi kuwa ya sauti mno mpaka nashindwa kusikia hata anayojibu. Naomba mpunguze mazungumzo. Mheshimiwa Naibu Waziri endelea.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, usanifu wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Machi 2009.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Ifakara una Mamlaka ya Maji iliyoanzishwa mwaka 2005 na kulingana na taratibu za uendeshaji Mamlaka iko katika daraja C.

Kiutaratibu, Mamlaka za maji za Makao Makuu ya Wilaya na Miji midogo zilizo katika daraja C, bado zinalipiwa gharama za umeme na Serikali kupitia Halmashauri za Wilaya zake hadi hapo zitakapoweza kujitegemea. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kulipa gharama za umeme zinazotumika katika kusuma maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Mlimba hauna Mamlaka ya Maji. Hivyo, huduma za maji katika mji huu zinaendeshwa na kampuni ya maji. Kampuni hii ndiyo inayohusika na ulipaji wa gharama za umeme unaotumika kuendesha pampu za maji.

Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero, inapaswa kutenga fedha katika Bajeti yake kwa ajili ya uendeshaji wa huduma za maji ikiwemo gharama za umeme wa kuendesha pampu za maji.

Serikali itaendelea kuboresha huduma ya maji kwa kupanua na kujenga miundombinu ya maji katika Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo hadi hapo miradi hiyo itakapoweza kujiendesha yenyewe.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika mji wa Mlimba kabla ya kampuni ya maji kuchukua kazi hiyo, kulikuwa na kampuni iliyojenga Mgodi wa Kihansi ndio ilikuwa inaendesha shughuli za maji. Na kulikuwa na kipindi cha mpito kati ya kampuni ya Mgodi wa Kihansi kuacha shughuli hiyo na Kampuni ya wananchi kuchukua shughuli za uendeshaji wa shughuli za maji. *(Makofi)*

Sasa kipindi hicho cha mpito kimeacha deni la takribani shilingi milioni 107 hivi, ambalo wananchi katika kampuni yao hawawezi kulilipa. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuwasaidia wananchi hawa kwasababu sio kosa lao? Kwamba deni hilo lifutwe au lilipwe na Serikali?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyoshauri katika jibu letu la swali la msingi kwamba Halmashauri ione inawezaje kusaidia mji mdogo wa Mlimba katika malipo yake ya umeme kwa huduma za maji basi vilevile hili suala lifikishwe katika Halmashauri na bila ya shaka Halmashauri italifikisha Serikalini na sisi tutaliangalia kwa sura hiyo.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tatizo la Ifakara linafanana kabisa na tatizo la Mpanda kwamba tunapata maji kwa kutumia pampu zinazoendeshwa kwa umeme ambazo tuna tatizo kubwa sana la kupatikana kwa umeme. Sasa hivi mashine zikiwa ni mbovu. Na uko mpango wa maji ya mtiririko kutoka Ikorongo, Serikali inasema nini kuhusu mradi huu wa maji ya mtiririko kutoka wa Ikorongo?

**NAIBU SPIKA:** Najua swali la nyongeza likiwa *very specific* na eneo fulani na yeye hakujiandaa, usishangae usipojibiwa. Lakini najua huyu ni fundi naomba ujibu Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa naibu Spika, kama tulivyosema hapo nyuma ni kwamba Mheshimiwa Waziri, mwezi Julai alitoa kauli kuhusu utekelezaji wa miradi ya vijiji 10 unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Na akipata nafasi tena katika kipindi hiki, katika mkutano huu, atatoa kauli nyingine; ikishindikana basi labda mkutano mwingine.

Lakini nilitaka nimwambie Mheshimiwa Arfi kwamba mipango yote ya maji inaanzia pale Wilayani na pale kama wakiona kwamba mradi huu wa mtiririko ni mradi ambao ni kipaumbele kwao, basi unaingizwa katika mipango ya maendeleo ya maji na hatimaye unaingizwa katika programu zinazoendelea.

Kwa hiyo, tutaliangalia suala la mradi huo, kama ni mpya kabisa tutauangalia katika miradi mingine lakini kama limo maana mimi sina hakika. Sasa hivi siwezi kulikumbuka kichwani, basi litajumuishwa katika programu hii ambayo inaendelea hivi sasa. (Makofi)

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa miradi inayofadhiliwa na Benki ya Dunia katika Halmashauri za Wilaya awamu ya kwanza na ya pili vimekwenda vizuri na miradi mingi ilitekelezwa. Na kwa kuwa, miradi ya awamu ya tatu haijaanza kutekelezwa na Mheshimiwa Naibu Waziri, alikwishatuahidi kwamba hii miradi itaanza kutekelezwa hivi karibuni. Na kwa kuwa, hivi sasa wananchi wanasubiri kwa hamu miradi hii kwa sababu wana matatizo makubwa ya maji ikiwemo wilaya ya Mpwapwa.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri ana maelezo gani kuhusu utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa na Benki ya Dunia awamu ya tatu?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyokuwa akijibu swali la nyongeza lililopita Mheshimiwa Naibu Waziri, amelitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa ruksa ya Spika, nikipangiwa nafasi kabla ya Bunge halijaahirishwa basi nitatoa kwa niaba ya Serikali, kauli ya Serikali kuhusu suala zima la Mpango wa Maji Safi na Usafi wa mazingira Vijijini, ikiwa ni pamoja na suala la miradi inayofadhiliwa na Benki ya Dunia.

Naomba avute subira, lakini kwa kuwa bila shaka nia yake ni kujua Mpwapwa kinafanyika nini. Basi, vilevile namtaarifu kwamba nimepanga ziara ya kwenda Mpwapwa kesho. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, fuata utaratibu wa kuomba hilo kwa sababu Bunge linakaribia kufika mwisho. Tunaenda Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa.

Na. 101

**Maandamano Haramu ya Zanzibar na Fidia**

*(Swali lililotajwa hapo juu liliondolewa na Muuliza Swali)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa kuokoa muda. Tunaenda swali la, Wizara hiyo hiyo lakini sasa namwita Mheshimiwa Paschal Degera. Wewe na mdogo wako mnaondoa maswali, kulikoni? *(Kicheko).*

Na. 102

**Kituo cha Polisi Kwamtoro Kupatiwa Gari**

**MHE. PASCHAL C. DEGERA** aliuliza:-

Kwa kuwa kituo kidogo cha polisi cha Kwamtoro Wilayani Kondoa kinahudumia eneo lenye matukio mengi ya mauaji na ujambazi na kwamba gari la kituo hicho ni bovu sana na halifanyi kazi kwa muda mrefu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukipatia kituo hicho gari jipya ili kuboresha utendaji kazi wa askari?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** Alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kituo cha polisi Kwamtoro kwa sasa hakina usafiri. Kwa hivi sasa kituo hicho kinapata huduma ya gari la Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Kondoa. Gari hilo pia ndilo linalotoa huduma kwa vituo vyote vya Wilaya ya Kondoa vikiwemo vituo vya Kwamtoro yenyewe, Bereko, Mrijochini pamoja na kituo cha Kondoa Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inatambua umuhimu wa kukipatia kituo cha polisi cha Kwamtoro vitendea kazi ikiwemo gari na pikipiki.

Hata hivyo uhaba wa Bajeti ya Wizara yangu unafanya utekelezaji wa kukipatia kituo hicho gari jipya kuwa mgumu. Tutajitahidi kutatua tatizo hili ambalo lipo katika agenda yetu.

Tatizo letu kubwa katika utekelezaji wa kupata vitendea kazi ni uhaba wa Bajeti, tutajitahidi kuona kwamba jitihada zinafanyika kuhakikisha kwamba haya yanatimilika.

**MHE. PASCAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali, la nyongeza aidha, namshukuru Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa gari moja kwa ukubwa wilaya ya Kondoa na wingi wa vituo vya polisi alitoshelezi kuweza kuhudumia maeneo yote kwa wakati mmoja na kwa kuwa katika jibu la msingi amesema kwamba kuna uwezekano wa kupata pikipiki na amekiri kwamba kuna ufinyu wa Bajeti.

Je, Wizara haiwezi kuangalia kwa utaratibu wa kupata pikipiki kwa ajili ya vituo vidogo vya kwa Mtoro, Mrijo Chini na Bereko.

Swali la pili kwa kuwa katika swali la msingi nimesema hivi kuna gari bovu pale kwenye kituo kidogo cha kwa Kwamtoro cha polisi. Je, haioni kwamba kuwa gari lipo hawezi kulitengeneza hilo gari liweze kuhudumia kituo cha polisi kwa Kwamtoro?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la kwanza kweli nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hali ya eneo lake tunalifahamu na tunazingatia na kila jitihada zitafanyika. Kusema kweli ahadi ya kusema kwamba gari linaweza likapatikana nashukuru kuona kwamba hata yeye ameliona nataka nimhakikishie kwamba tutafanya kila jitihada kwa kuzingatia ukubwa wa eneo tuone kwamba wanaweza wakapata pikipiki.

Kuhusu gari ambalo analitaja ni kweli lipo gari *STG 3686* pia liko jingine pia *TZR* ambalo hilo hilo lina namba ya TZR 6516 tumeomba kutoka kwa *RPC* tupate makadirio ya gharama za kuweza kulitengeneza hilo gari na hivi wakati tunaandaa hili jibu lake jana nimepata makadirio wanatuambia kwamba itakuwa takribani milioni sita kulitengeneza hilo gari.

Kwa hiyo, ningeomba kwamba tujaribu kutizama kama kutengeneza hilo gari itakuwa kweli inakwendana na hiyo milioni ama tunaweza tutatizima lakini nataka kumwambia kwamba tumeweza kupata gharama ambayo itakuwa ni kiasi cha milioni sita. Kwa hiyo, hebu tajaribu kutizama kama uwezekano unaweza kuwepo tuweze kulitengeneza hilo gari.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa niulize swali moja tu la nyongeza kwa vile matatizo haya ya usalama yanayotokea kwa Mtoro Kondoa yanafanana kabisa nay ale yanayotokea Kibaigwa katika wilaya ya Kongwa ambalo ni soko kubwa la kimataifa la nafaka ambapo ni mji mdogo wenye soko la kimataifa la nafaka lakini hakuna kituo cha polisi, kituo wananchi walikwishajenga miaka mingi na nimekuwa nikisema kila mwaka hapa Bungeni kwamba pale mahali panahitaji ulinzi wa polisi, panashindikana hata kujenga mabenki kwa sababu hakuna polisi pale. Sasa na Wizara mara zote imeahidi kwamba kituo kile kitazinduliwa polisi watawekwa pale lakini haifanyiki hivyo.

Swali langu ni kwamba Je, Mheshimiwa Naibu Waziri au Waziri mwenyewe atakubali anapotoka Bungeni hapa kupita Kibaigwa pale kujionea mwenyewe kituo kilichojengwa na wananchi ili sasa suala hilo la kuweka askari likatekelezeka?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimekubali siku tutakapomaliza kikao cha Bunge kesho yake tutaenda na Mheshimiwa Mbunge kwenda kukagua eneo na kuangalia uwezekano wa kupeleka polisi na kufungua kituo. (*Makofi*)

**MHE. FATUMA O. ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuwa suala la wilaya ya Kondoa si tofauti na suala mazingira ya mkoa wa Mjini Magharibi Zanzibar. Je, Waziri atalieleza lini Bunge kupatiwa kituo cha polisi Mazizini gari la kufanyia doria?

**NAIBU SPIKA:** Ndiyo yale yale mkianza kuita mahali maalum itakuwa tatizo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi mwenyewe takribani kiasi mwezi umepita nilikuweko Zanziar Mjini Magharibi na niliona hali halisi ilivyo na tulizungumza na viongozi wa pale, *RPC* alikuwepo. Kwa hiyo, hili tatizo ambalo analizungumza Mheshimiwa Fatuma si tatizo ambalo linahusu sehemu moja tu. Ni tatizo ambalo tunalo Tanzania nzima na kwa kweli kila jitihada zinafanyika kuona siwezi nikaahidi hapa kusema kwamba gari tutaweza kukuleteeni, sababu mnazifahamu Waheshimiwa Wabunge hali ya Bajeti yetu ilivyokuwa tatizo. Lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Fatuma kwamba ombi lake tumelizingatia.

Na. 103

**Mkandarasi wa Ujenzi wa Barabara ya Babati Hadi Simanjiro na Kiteto**

**MHE. OMAR S. KWAANGW'** aliuliza:-

Kwa kuwa wakati wa kuanzisha Mkoa wa Manjara ilitolewa ahadi ya kuijenga barabara ya kudumu kutoka Babati kuelekea Wilaya ya Simanjiro na Kiteto:-

(a)Je, ni fedha kiasi gani amelipwa Mkandarasi kwa awamu zote mbili kati ya Singe – Gedamar hadi Kimotorok?

(b)Je, Mkandarasi huyo alichukuliwa hatua gani pale alipoonekana kuwa amekiuka mkataba kwa kushindwa kumalizia kazi kwa wakati?

(c)Je, sehemu ya barabara kutoka Kimotorok kuelekea Kibaya amepewa Mkandarasi gani na mkataba wake utagharimu kiasi gani cha fedha?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omar Shaban Kwaangw', Mbunge wa Babati Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kazi ya kuifanyia matengenezo barabara ya Singe- Gedamar hadi Kimotorok yenye urefu wa kilometa 80.4 ilikabidhiwa kwa Mkandarasi *Wesons Tanzania Ltd* kwa mikataba mitatu.Katika mwaka wa fedha 2004/2005, sehemu ya kwanza ya Singe – Gedamar yenye urefu wa kilometa 17.5 ilitekelezwa kwa gharama ya shilingi 760,180,787. Katika mwaka wa fedha 2005/2006 sehemu ya pili yenye urefu wa kilometa 5.0 ilitekelezwa kwa gharama ya shilingi 361,284,656. Mkandarasi alikamilisha kazi katika awamu zote mbili na hivyo kulipwa jumla ya shilingi bilioni 1.1.

Katika mwaka 2006/2007 sehemu ya tatu ya Gedamar – Kimotorok yenye urefu wa kilomita 57.9 ilipangwa kutekelezwa kwa gharama ya shilingi bilioni 1.3. Mkandarasi alishindwa kumaliza kazi hiyo na hivyo mkataba kusitishwa. Katika mkataba huo mkandarasi alilipwa shilingi milioni 744.58 ikiwa ni asilimia 57 ya mkataba wote.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mkandarasi kuonekana anachelewa kukamilisha kazi kulingana na ratiba iliyopo kwenye mkataba, mwajiri alimwonya na kumtaka aongeze kasi ya utendaji. Pamoja na onyo mkandarasi aliendelea kusuasua na kutofanya kazi yake vizuri hivyo mwajiri kulazimika kumkata fedha kiasi cha shilingi milioni 130.67 kwa kuchelewa kazi kulingana na mkataba. Hata baada ya hatua hiyo kuchukuliwa, mkandarasi aliendelea kusuasua katika utendaji wa kazi. Baada ya mwajiri kufuata taratibu zote za kimkataba za kumwonya mkandarasi bila mafanikio. Tarehe 28/10/2008 mwajiri alimfukuza kazi rasmi.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa barabara kutoka Kimotorok kuelekea Kibaya/Simanjiro yenye urefu wa kilometa 64.5 unatekelezwa na Mkandarasi *M/S Nyakirang'anyi Contruction Co. Ltd.* Kwa gharama ya shilingi bilioni 1.46. Mkataba ulianza Aprili, 2008 na umepangwa kukamilisha Machi 2009. Hadi sasa Mkandarasi amekamilisha kazi ya matengenezo kwa asilimia 40 na kulipwa jumla ya shilingi milioni 310.346 sawa na asilimia 21.3 ya gharama za mkataba.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru naomba niulize maswali mawili kama ifuatavyo. Kwanza Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba mkataba huu wa awamu ya tatu Gedamar Kimotorok ilikuwa bilioni 1.3 na mkandarasi amelipwa milioni 700 kwa hesabu zangu za haraka inaonyesha kwamba tumepata hasara ya shilingi milioni 562 ambayo ni zaidi ya milioni nusu bilioni na kwamba kazi imekamilika kwa asilimia 57 tu kwa hiyo bado asilimia 43. Je, sasa Serikali ina mpango gani kukamilisha hii asilimia 43 kwa kuweka mkandarasi mwingine?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hasara ya nusu bilioni na mkandarasi kutozwa zaidi ya shilingi milioni 130. Je, kazi hiyo sasa ambayo itakamilishwa ya asilimia 43 itaigharimu Serikali kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kazi iliyobakia ambayo haikutekelezwa na yule mkandarasi aliyesimamishwa kazi ambayo ni asilimia 43, tathimini ya kazi hiyo iliyosalia sasa imefanyika ambayo awali ilikuwa ikijengwa na hiyo kampuni ya *Weasons. K*wa hiyo, tenda sasa hivi ya ujenzi huo imeshatagazwa na inatarajiwa mwezi huu wa Februari, itafunguliwa na wakati huo tukishakuwa tumeshafungua kandarasi hiyo na gharama zake zitafahamika.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa wakati wa kuunda mkoa huo wa Manyara, Rais wa wakati huo Mheshimiwa Benjamini Mkapa aliwaahidi wananchi wa Simanjiro kwamba barabara hiyo itatengenezwa kwa kiwango ambacho kitapitika kwa wakati wote. Kwa kadri ya fedha zinazotengwa kila mwaka fedha hizo hazitoi matumaini kwa zaidi ya miaka 16 ili iweze kupitika?

Je, Serikali inawaahidi nini sasa wananchi hao kwa kutengeneza fedha zinazoweza kukidhi kuunganisha makao makuu ya wilaya ya Simanjiro na makao mkuu ya mkoa ya wilaya ya Kiteto na makao makuu ya mkoa?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika majibu yangu ya msingi hapa nimeeleza kwamba ile sehemu ya barabara hii ya kuunganisha mpaka Simanjiro mkandarasi tayari ameshateuliwa na kiasi kinachogharimiwa kwa hakika barabara hiyo nimeelezwa kuwa ni shilingi bilioni 1.46.

Nataka nilihakikishie Bunge lako Tukufu kuwa barabara hii nimeipita hivi karibuni. Kazi za ujenzi wa barabara hii zinaendelea vizuri na tunaendelea kuzingatia kutenga fedha kwa kadri itakavyokuwa inawezekana ili barabara hii ikamilike kama alivyokuwa ameahidi Mheshimiwa Rais wa awamu ya tatu.

Na. 104

**Kupeleka Kivuko Mitomoni Katika Mto Lunyele**

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, sasa Serikali imeweka kivuko cha kisasa katika Mto Ruhuhu na kinafanya kazi vizuri, na kwa kuwa, kabla ya kivuko hicho kulikuwa na kivuko cha kusukuma kasia na kamba ambacho kimebaki pale pale kivukoni:-

(a) Je, Serikali haioni vema kukipeleka kivuko hicho Mitomoni Wilaya ya Mbinga kwenye mto Lunyele ili kisaidie kuvusha watu badala ya kukiacha bila matumizi?

(b) Kama itakubalika hivyo, je kazi hiyo itafanyika lini?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Capt. John D. Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi, swali lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba katika mto Ruhuhu kuna kivuko cha kutumia kamba ambacho hivi sasa hakitumiki baada ya Serikali kuweka kivuko cha kisasa katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa Mheshimiwa Mbunge wa kukipeleka kivuko hicho Mitomoni katika mto Lunyele tumeupokea. Wizara itatuma wataalamu kuona kama kivuko hicho kinafaa kufanya kazi katika maeneo hayo pamoja na kuangalia pia gharama halisi ya kuhamisha kivuko hicho na maegesho yake ili kufanya uamuzi wa kutekeleza ombi la Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, iwapo taarifa ya wataalamu itaonyesha kuwa kinaweza kufanya kazi katika eneo hilo, kazi ya kuhamisha kivuko hicho itafanywa baada ya kutenga fedha katika Bajeti ya Mwaka 2009/2010.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Naibu Waziri nina maswali mafupi mawili ya nyongeza.

1. Pamoja na kwamba Serikali inasema itatuma wataalam kwenda kuangalia sehemu hiyo, ombi langu nilikuwa naomba je, Serikali inaweza kuniambia ni lini hasa hawa watakwenda na mimi niongozane nao?

2. Ile pantoni ambayo imewekwa ya kisasa pale sijui kama Serikali inajua kwamba kapteni wa meli ile au patoni ile ametoweka karibu miezi miwili iliyopita na huduma hiyo haifanyiki na kama inafahamu atapelekwa kapteni mwingine pale?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza juu ya lini wataalam hao watakwenda, nataka tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaandaa taratibu za wataalam hao kwenda. Kwa hiyo, tutakapokuwa tumekubaliana tarehe mahususi kwa sababu Mheshimiwa Mbunge anataka kufuatana nao tutamfahamisha. *(Makofi)*

Lakini hili la pili la kwamba kapteni wa pantone ametoweka taarifa ndiyo tunaipata sasa hivi, nataka tu niseme kwamba tumeipokea na tunaifuatilia ili kuweza kufanyia marekebisho eneo hilo liweze kufanya kazi vizuri.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa vile matatizo ya pantoni ya mto Ruhuhu kwenye eneo hilo yanasababishwa zaidi na mto Ruhuhu kutokuwa na kina wakati wa kiangazi, ndiyo maana hata kivuko cha zamani sana bado kimefukiwa kwenye tope hakijafukuliwa mpaka leo pale. Je, kwa vile inaonekana vivuko pale havifai Wizara hii inaweza ikashirikiana na Wizara ya Maji na Umwagiliaji wajenge sasa daraja pale kwenye mto Ruhuhu badala ya vivuko ambavyo havifai pale?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutatua utatuzi wa maeneo haya ya majini kwa kutumia vivuko ambavyo Mheshimiwa kasema katika maeneo ya mto huo hayafai kwa kweli suluhisho la mwisho lingekuwa ni kujenga daraja. Kwa kweli itakuwa ndiyo suluhisho la mwisho.

Lakini sasa kikubwa zaidi hapa ni uwezo wa Serikali kuweza kutekeleza miradi hii ya ujenzi wa madaraja. Lakini hata hivyo naomba tulichukue kama ni ombi, tutaendelea kulifanyia kazi kwa kadri ya uwezo wa Bajeti utakavyokuwa unaruhusu, tutalitekeleza hatua kwa hatua. *(Makofi)*

Na. 105

**Shule za Sekondari Kupatiwa Vitendea Kazi**

**MHE. RICHARD M. NDASSA** aliuliza:-

Kwa kuwa, baadhi ya shule za sekondari za Serikali hapa nchini hupatiwa magari au pikipiki kama vitendea kazi.

(a)Je, ni sifa gani zinazofanya baadhi ya shule kupata vitendea kazi na zingine zisipate?

(b)Je, shule za Sekondari za *Sumve Girls* na Talo Sekondari hazistahili kupata vitendea kazi hivyo na kama zinastahili zitapata lini?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA**) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Richard Ndassa, Mbunge wa Sumve, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nia ya Serikali ni kuhakikisha kuwa kila sekondari inakuwa na gari ili liweze kutoa huduma mbalimbali. Hata hivyo kutokana na ufinyu wa Bajeti si rahisi kwa kila shule ya sekonari kupatiwa gari.

Wizara imeifanyia kazi suala la shule ya sekonari ya Sumve na tutaliingiza katika Bajeti ya mwaka 2009/2010. Hivyo tunamwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeridhika na majibu ya Serikali, ahsante sana.

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni Serikali imetoa maelekezo kwamba wazazi wakalipie kwenye benki ada kwa sekondari za Kata na hali hiyo inasababisha gharama kubwa kwa wazazi na kama anakwenda

kulipia Shilingi 10,000/= inabidi atumie hela Shilingi 10,000/= zingine kwa ajili ya nauli pamoja na kujikimu.

Je, Serikali haioni kwamba uamuzi huu siyo wa busara sana unawaumiza wananchi hasa wazazi. Je, isingewabana tu walimu wakuu wanaokula fedha za ada wazilipe ama wachukuliwe hatua za kinadhamu? Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dr. Limbu swali hili kabisa kabisa halifanani na *original one*. Kwa sababu ya *interest* naomba ujibu tu. Lakini halifanani kabisa huyu alikuwa anauliza gari la shule.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba niseme ni utaratibu wa Serikali na ndiyo Kanuni za fedha kwamba zikalipwe benki ni kwa usalama wa fedha zenyewe. Lakini ni kwa usalama wa wakuu wa shule. Si jambo jema kutangazia umma kwamba wakuu wa shule wanakusanya fedha na hasa kwa baadhi ya Mikoa hiyo anayotoka yeye walimu kadhaa wameshapoteza maisha kwa ajili ya kuwa na taarifa ambazo si sahihi kwamba wanazo kiasi kikubwa cha fedha majumbani.

Kwa hiyo, naomba niseme kama katika eneo analotoka Mheshimiwa Mbunge yapo matatizo basi watumie vikao vya Bodi kuweza kutafuta namna nzuri ambayo wazazi watalipa hizo fedha na kuwaondolea usumb ufu. Swali lake jingine ambalo limekuja (a) na (b) ya kwamba tuwabane walimu wakuu wanaokula fedha, naomba tuweke imani kwa hawa walimu wakuu tunawaamini wanafanyakazi katika mazingira magumu. Wanastahili kuheshimiwa wachache ambao siyo waadilifu tupatiwe taarifa zao, tutawachukulia hatua za kinidhamu. (*Makofi*)

**MHE. VEDASTUS MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Sambamba na mahitaji ya vitendea kazi kama magari katika shule hizi, lakini vile vile kuna tatizo kubwa la fedha za ukarabati hasa katika shule kongwe. Ningependa kujua ni lini Serikali itaanza kutoa fedha za ukarabati kwa ajili ya shule kongwe zikiwemo shule ya Sekondari ya Mara, pamoja na *Musoma Tech?*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ikumbukwe kwamba katika hotuba ya Bajeti ya mwaka 2008/2009 Waziri mwenye dhamana alieleza bayana kwamba tutazikarabati shule kongwe zote kwa awamu na kwamba mwaka 2007/2008 shule 30 zilikuwa kwenye mpango na mwaka 2008/2009 ziko tena nyingine kwenye mpango. Shule hizi ni nyingi na ziko kwenye mpango Musoma na Mara ziko katika mpango. Naomba tu kadri tutakapopata fedha za maendeleo tutazipelekea fedha hizo kwa ajili ya ukarabati. Tunatambua, tunafahamu tutazifanyia ukarabati. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru kwa kujibu maswali ambayo hayamo kwenye swali la nyongeza.

Na. 106

**Mpango wa Kuongeza Upatikanaji wa Elimu ya Juu Nchini**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA (K.n.y. MHE. PINDI H. CHANA**) aliuliza:-

Kwa kuwa, elimu ndio msingi wa maisha hasa katika nyakati hizi za dunia ya utandawazi?

(a) Je, Serikali ina mkakati gani ya kuhakikisha kuwa elimu ya juu inakuwa ni ya lazima kwa kila Mtanzania?

(b) Je, ni asilimia ngapi ya Watanzania wenye umri na uwezo wa kupata elimu ya juu wanapata?

(c) Je, ni changamoto zipi zinazoikabili Serikali katika kufikia asilimia 90 (90%)?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA C. KABAKA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu a, b, na c kama ifuatavyo:-

(a) Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa elimu ndiyo msingi wa maisha na hasa katika nyakati hizi za dunia ya utandawazi. Serikali kwa sasa haina mpango wa kuhakikisha kuwa elimu ya juu inakuwa ni lazima kwa kila Mtanzania. Hii ni kutokana na gharama kubwa za uendeshaji wa elimu ya juu na uwezo wetu mdogo kiuchumi. Hata hivyo pamoja na uwezo mdogo wa kiuchumi wa nchi yetu, Serikali imeweka mikakati mbalimbali ya kuhakikisha kuwa Watanzania wengi wanapata elimu ya juu. Mikakati hiyo ni pamoja na kupanua Vyuo vya Elimu ya Juu kwa kushirikisha sekta binafsi na kuongeza idadi ya wanafunzi vyuoni.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, wastani wa asilimia 55 ya Watanzania wenye umri wa maika kati ya 20 -23 hujiunga na Vyuo vya Elimu ya Juu baada ya kuhitimu kidato cha sita na kupata daraja la I – III. Hii ni idadi ndogo sana ukilinganisha na idadi ya vijana wa umri rika (*cohorts*). Kwa sasa inakadiriwa kuwa ni asilimia 3.8 ya vijana wenye umri wa kwenda Vyuo vya Elimu ya Juu hupata elimu hiyo.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa zinazoikabili Serikali katika kuongeza upatikanaji wa elimu nchini ni uwezo mdogo wa Serikali wa:-

- Kutenga Bajeti ya kutosha kwa taasisi za elimu ya juu.

- Kukarabati miundombinu ya Vyuo vya Elimu ya Juu iliyochakaa na kuongeza nafasi ili kukidhi mahitaji.

- Kuwepo upungufu wa wanataaluma, vyumba vya maabara, vifaa vya kufundisha na kujifunzia.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Pamoja na majibu hayo mazuri na changamoto ambazo amezizungumzia. Naomba nitoe swali moja la nyongeza. Kwa kuwa katika siku za karibuni katika Vyuo vya Elimu ya Juu hususani watoto wa kike wamekuwa wakipata matatizo makubwa hasa pale inapotokea vyuo hivyo vinafungwa na kusababisha wao kujihifadhi katika nyumba ambazo zipo jirani na vyuo na pengine kujiingiza hata katika vitendo visivyostahili na kuwaletea hatari hata ya kupata ujauzito. Sasa ili kuweza kujua wanafunzi hao hasa hao wa kike ambao ni taifa la kesho wanakabiliwa mambo yepi au changamoto zipi?

Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba ni vema sisi kama wazazi akaunda Kamati ndogo ikijumuisha yeye mwenyewe na Waheshimiwa Wabunge wachache na wengine wana taaluma ili kuweza kuongea na hao watoto wa kike kuweza kusikia changamoto zao?. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA C. KABAKA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, kwa uchungu wake kuhusu elimu na hasa elimu ya mtoto wa kike. Siyo nia ya Serikali kwamba hao watoto hasa wakike wabakie Dar es Salaam au mijini wakati vyuo vinapofungwa baada ya fujo ambazo huwa zinatokea katika vyuo vyetu vikuu. Inapokuwa imetokea fujo na Vyuo Vikuu vimefungwa ni matarajio ya Wizara na vyuo vyenyewe ni kwamba wanafunzi hawa wanarudi majumbani kwa wazazi wao na walezi wao. Kule watasubiria hatima ya kurudi kwao katika vyuo wakati huo wakiwa wanawasaidia wazazi wao, wakifanya shughuli zingine za kijamii huko huko walikozaliwa au wanakoishi. Kwa hiyo, kama wanabakia mijini hiyo ni nje na matarajio ya Wizara na nje ya matarajio ya jamii. Kwa hiyo, naomba hiyo isitokee.

Lakini kwa suala kusikiliza changamoto zao mimi nakubaliana na Mheshimiwa Stella Manyanya na niko tayari kuungana naye na akina mama wengine ambao wangependa kuwasikiliza hao wanafunzi wa kike kwasababu kwa kweli kutokana na mahitaji yao maalum na kutokana na hali halisi ya mtoto wa kike katika vyuo na Taasisi zingine za Elimu ya Juu najua watakuwa na changamoto ambazo ni tofauti na za vijana wa kiume. Niko tayari kuungana na wanaopenda kufanya hivyo kuwasikiliza wanafunzi hawa ili waweze kusoma kama wengine katika vyuo vikuu. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN ANSELM JEROME LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa swali la msingi linahusu umuhimu wa kuongeza idadi ya wanafunzi katika vyuo vya elimu ya juu, na kwa kuwa hata wachache waliopo wanasoma katika mazingira magumu sana ikiwa ni pamoja na miundombinu mibovu, upungufu wa

wahadhiri pamoja na mambo mengine mengi ambayo yamepelekea Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambacho ni chuo chetu cha kihistoria kuporomoka kutoka katika nafasi ya 13 kwa ubora katika vyuo vya Afrika mwaka juzi hadi nafasi ya 27 mwaka jana 2008.

Je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha kwamba wale wanafunzi wachache waliobahatika kusoma katika vyuo vya elimu ya juu hawapati vikwazo visivyo na msingi kwa mfano wanafunzi wale 600 ambao wamekata rufaa mpaka sasa hivi bado hawajarudi vyuoni? Aidha niliomba kabisa wanafunzi hao wakati rufaa zao zinashughulikiwa wawe vyuoni kwa maana ya wiki tatu zikipita wanafunzi wale watakuwa wamejifukuzisha chuoni.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo, tena swali lako ni moja tu.

**MHE. SUSAN ANSELM JEROME LYIMO:** Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba walau wale wanafunzi 600 wanarudi chuoni ili ile nafasi yao isiweze kufutika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri unajibu kipande cha kwanza tu kwa sababu swali ni moja.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA MUGOSI KABAKA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu sehemu ya kwanza ya swali la nyongeza la Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo, kama ifuatavyo:-

Kama tulivyosema katika jibu letu la msingi, tunakubaliana na Mheshimiwa na Mbunge Pindi H. Chana, kwamba kikweli miundombinu ya Vyuo Vikuu imeharibika na tumesema hii ni kutokana na uwezo mdogo wa Serikali kwamba hatuwezi kutoa pesa za kutosha kila mara kutengeneza miundombinu hii na kuiweka katika hali nzuri ya kusomea.

Lakini hata hivyo, katika Bajeti ya mwaka huu tumetenga pesa kwa ajili ya ukarabati wa baadhi ya miundombinu na Mamlaka ya Elimu Tanzania imetoa pesa kukarabati baadhi ya miundombinu hiyo ikiwa ni pamoja na ile *lift* iliyokuwa imeharibika pamoja na vyoo.

Mheshimiwa Waziri mwenyewe pamoja na mimi tumetembelea Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Mzumbe, pamoja *SUA* na kujionea hali halisi na tuna pesa za *Quick Wins* ambazo pia tunazipeleka hivi karibuni vyuoni ili kutengeneza miundombinu hii.

Kwa hiyo, Serikali inajitahidi na pia inajitahidi kuajiri wahadhiri wa kutosha wengi wanaomaliza masomo tunawabakiza, tunawakopesha ili waweze kusoma na kuendelea kufundisha katika vyuo hivi vikuu.

Naomba tukubaliane kwamba Serikali inajitahidi na inatambua umuhimu wa elimu ya juu pamoja na kwamba tumesema siyo elimu lazima kwa kila Mtanzania.

**MHE. ESTHER KABADI NYAWAZWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na hatimaye sasa na mimi umenipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali yetu ya Chama Cha Mapinduzi ya kuhakikisha kwamba imejenga Chuo Kikuu Dodoma na Serikali kwa kweli ina uwezo wa kuamua maamuzi yake na yakatekelezeka. (*Makofi*)

Sasa baada ya Chuo Kikuu cha Dodoma Serikali tuna mpango gani tena wa kujenga chuo Kikuu kikubwa hivyo hivyo katika Kanda ya Ziwa?

**NAIBU SPIKA:** Swali hili ni lingine kabisa.

Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na tunaendelea na shughuli nyingine.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA :** Mwongozo wa Spika!

## MWONGOZO WA SPIKA

**NAIBU SPIKA:** Spika akisimama wewe unakaa na Spika akikaa wewe unasimama. (*Kicheko*)

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako. Kwa kuwa, mbunge yeyote anaruhusiwa kuliondoa swali kwa mujibu wa Kanuni ya 41(b) lakini kwa kuwa vilevile ikiwa Waziri mhusika alijiandaa na jibu na Mbunge akiliondoa swali ina maana lile jibu Wabunge wengine wamelikosa kulisikia na wakati wengine tunalihitaji lile jibu.

Je, tufanye nini ili kulipata jibu la Waziri aliyetaka kulijibu swali lile ? (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge kama una haja kabisa na swali lile unakwenda kulinakili kama lilivyo na unaandika jina lako halafu utajibiwa kwa sababu mwenye swali inawezekana kabisa huko nje amezungumza na wanaohusika akaridhika. Kwa hiyo ana mamlaka ya kuondoa swali lake ninyi wengine siyo maswali yenu mpaka yule anayeuliza ndiyo maana tunamtaka yule anayeuliza aulize na maswali mawili ya nyongeza. Sasa maswali yenu mpaka yule anayeuliza ndiyo maana tunamtaka yule anayeuliza na tunampa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Sasa amesema anaondoa swali lake, ni uamuzi wake.

Lakini kama wewe bado unalifikiria lile swali ungetamani majibu haizuii tena na wewe ukalinakili tena ukabandika jina lako ukalipeleka, haizuii kabisa. (*Makofi*)

Waheshimiwa wabunge, ukiwa na Wajumbe wa mkutano kama huu 300 na zaidi inakuwa rahisi kuendesha kama Kanuni zinafuatwa na mnazifahamu kwa sababu tukienda kama nilivyojifunza leo unakuta mtu anasimama swali la nyongeza ambalo siyo lake. Analeta swali lingine kabisa na vijiji vingine kabisa. Mawaziri hawawezi kujua kila kijiji katika vijiji vyote vya nchi hii. Unaweza kuuliza swali la kiujumla la kisera. Sasa Waziri pale kijumla ni lazima afahamu lakini kujua kijiji cha kwangu kinaitwa kwa jina fulani. Kwa kweli unataka kutupotezea muda wetu kwa sababu Waziri hatakutendea haki kwa sababu wewe hukumtendea haki Waziri yule. *(Makofi)*

Lakini la pili, jamani mzingatie taratibu zetu, kwa mfano Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo, sasa hivi ametaka kujaza maswali mengi katika swali moja. Jamani tukumbuke tunawahutubia wananchi wote na dunia nzima.

Sasa mimi nakuambia ujibu sehemu ya kwanza tu, wananchi wanaonisikiliza wanafikiri mimi nimekukatili tu lakini Kanuni zetu zinasema anayeuliza swali la nyongeza kama si mwuliza swali atauliza swali moja tu.

Kwa hiyo, ndiyo maana nikasema atajibiwa swali lake sehemu ya kwanza tu na ninaomba tuzingatie Kanuni tutapata amani na tutapata furaha ya kuendesha Bunge letu vizuru. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wafuatao:-

Wageni wa Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI ni Wamerekani wanaojitolewa na Watendaji washiriki wa Kitanzania 24 wakiongozwa na Viongozi wa *P-Scopes* Tanzania ambao ni Alice Mtenga, Beatus Mwendwa na Francis Saria. *And we would like to see the P-Scopes if they are in the chamber. You can stand all together. You are welcome*. (*Makofi*)

Wageni 29 wa Mheshimiwa Felister A. Bura, ambao Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi, Dodoma wakiongozwa na Mwenyekiti wa UVCCM Dodoma Bwana Mwinje na Bwana Kitundu Katibu wa UVCCM Mkoa wa Dodoma. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, ambao ni Emmy Slaa mtoto wake ni mwanafunzi wa Chuo Kiuu cha Dar es Salaam. Karibu sana na ninakutakia kheri katika masomo. Kuna Dorine Kisamo anasoma Chuo Kikuu Dodoma, Dorine. Karibu sana. (*Makofi*)

Tuna mgeni pia wa Mheshimiwa Jenista J. Mhagama ambaye ni Padri Rogers Haule Paroko wa Ifinga Jimbo la Peramiho. Ahsante sana hata mimi namfahamu sana

alipopata Upadri mimi nilikuwa Mkuu wa Mkoa kule. Karibu sana Baba Paroko. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa ambao ni Margareth Kame Mwenyekiti wa Mtaa wa Mnadani Dodoma, Ndugu Aisha Kidile, Afisa Mtendaji wa Mnadani Dodoma. Karibuni sana tunafurahi kuwaona. (*Makofi*)

Halafu kuna wageni kutoka Ubalozi wa Marekani ambao ni *Carl Forks Head of Political and Economic Section* na *Tinna* Mdobilu *Political Assistant. You are welcome to Dodoma and hope to see you in the afternoon.* (*Makofi*)

Kuna wageni kutoka Ubalozi wa Uingereza ambao wanaendelea na ziara yao hapa Bungeni ambao ni John Brants, *Political Officer, Darine Wech Head of Department of International Development* na *Simon Gill, Head of Department of International Development* na *Charles Okine, Governance Advisor. So they were here yesterday and you are welcome again today.* (*Makofi*)

Wanafunzi 14 kutoka Chuo Kikuu Mzumbe, wako hapa Dodoma kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo katika ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Naomba wasimame pale walipo. Karibuni sana na tunawatakia mafunzo mema. (*Makofi*)

Wanafunzi wengine 28 kutoka *Dar Independent School* na Walimu wao. Karibuni sana. Nadhani wameondoka.

Waheshimiwa Wabunge, sina hakina na matangazo ya kazi wakati leu tuna mkutano ule lakini nitatangaza wenyewe watafahamu.

Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuwa kutakuwa na kikao cha Kamati leo tarehe 5 Februari, 2009 katika Ukumbi Namba 219 ghorofa ya pili jengo la Utawala saa kumi jioni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Alhaj Mohamed Hamisi Missanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya MIundombinu, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge ambao ni Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo tarehe 5 Februari, 2009 kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo katika ukumbi wa Mheshimiwa Pius Msekwa mara baada ya Mkutano uliopangwa chini ya Wizara ya Fedha utakapokwisha.

Waheshimiwa Wabunge, mimi ninadhani tukitoka katika mkutano ule wao wanaingia katika mkutano wao.

Mheshimiwa Wilson Mutagaywa Masilingi, ingawa sijaona *signature* yako katika tangazo hili.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje na Mambo ya Usalama anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo tarehe 5 Februari, 2009 katika Ukumbi Namba 231 Jengo la Utawala, mara baada ya mkutano uliopangwa chini ya Wizara ya Fedha utakapoahirishwa Waheshimiwa Wabunge wote wawasiliane.

Nilisahau, kulikuwa na wageni wa Mheshimiwa Janeth Mourice Massaburi, ambao ni Bi Iluminata Madaha na Bi Rukia. Hawa ni Walimu wa Ujasiriamali wa utengenezaji wa Chaki na Batiki. Kwa hiyo, hawa ni wataalamu wa mambo hayo. Karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa napenda kusema leo ni *Happy Birthday* ya Chama cha Mapinduzi. Kwa nini ninyi hampigi Makofi? Kwani hili ni tatizo? (*Makofi/Kicheko*)

Baada ya kusema hivyo, hili ni tangazo linalotuhusu wote. Baada ya kikao hiki sasa tunaondoka kwenda katika Ukumbi wa Mheshimiwa Pius Msekwa, tuna ule Mkutano wa kupewa Hali ya Uchumi katika nchi yetu.

Ni mkutano ambao Waandishi wa Habari pia wanakaribishwa. Kwa hiyo, hiyo ndiyo shughuli tutakayoifanya leo na Waheshimiwa Wabunge naomba wote mhudhurie kwa sababu yatakayozungumzwa yale ni muhimu kabisa katika Maendeleo ya nchi yetu.

Kwa hiyo, ni vizuri mkasikiliza kwa sababu wananchi watakwenda kuwauliza na ninyi mtasema hatuelewi! Kwa hiyo, mhudhurie na kusikiliza kikao kile kwa uzuri kabisa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo mimi sina tangazo lingine naomba kuahirisha kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. (*Makofi*)

*(Saa 7.00 Mchana Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa, Tarehe 6 Februari, 2009 Saa Tatu Asubuhi)*